# Mradi wa WOLTS Tanzania

# Muhtasari wa Ripoti--Mundarara

# Agosti 2017

Daley, E., Lanz, K., Mhinda, A., Driscoll, Z., Ndakaru, J.,
Grabham, J. na Kereri, E.



Muhtasari huu unajumuisha matokeo ya utafiti wa mradi wa WOLTS Tanzania – Ripoti ya kijiji cha Mundarara, Agosti 2017, inapatikana kwenye tovuti ambayo ni www.mokoro.co.uk/wolts.

Maandishi © Timu ya WOLTS. Picha zote © Timu ya WOLTS.

# Utafiti na mbinu za Mradi wa WOLTS

Mradi wa utafiti wa mpango mkakati wa muda mrefu unaofanywa na Mokoro kwa kushirikiana na HakiMadini "kutafiti changamoto za usalama wa umiliki wa ardhi kwa wanawake nchini Tanzania". Mokoro kwa kushirikiana na HakiMadini Tanzania, wamekuwa wakitafiti hali ya usalama wa umiliki wa ardhi kwa wanawake wa jamii za kifugaji zinaoathiriwa na uwekezaji wa uchimbaji madini kupitia njia shirikishi za utafiti ili kubaini changamoto/vikwazo mbalimbali vya haki za ardhi kwa wanawake na makundi maalumu. Mradi wa WOLTS unalenga kutathmini njia sahihi ya kuboresha usawa wa kijinsia katika umiliki na usimamizi wa haki za ardhi ili kulinda haki za umiliki wa ardhi kwa makundi maalumu dhidi ya vikwazo/changamoto katika jamii husika pamoja na kusaidia jamii kwa ujumla kuhimili changamoto juu ya ardhi na maliasili zao (angalia tovuti yetu www.mokoro.co.uk/wolts/).

Muhtasari huu unashirikisha matokeo ya utafiti wetu katika Kijiji cha Mundarara uliofanyika kati ya Septemba 2016 na Februari 2017, ikiwa ni pamoja na ziara za awali, utafiti wa awali na utafiti shirikishi. Tunawashukuru watu wote wa kijiji cha Mundarara kwa ushirki na ukarimu wao wakati wote wa utafiti na msaada mkubwa tuliopewa na Halmashauri ya Wilaya ya Longido.

Utafiti wa awali uliohusisha asilimia kumi (10%) ya nyumba katika vitongoji vyote vya kijiji cha Mundarara ulifanyika Oktoba 2016. Utafiti huo ulihusisha nyumba 71 kati ya hizo 57 zilichaguliwa bila kuzingatia sifa maalumu na nyumba 14 zilikuwa nyumba zinazoongozwa na wanawake. Hivyo 80% ya jumla ya sampuli ya utafiti ilichaguliwa bila kuzingatia sifa maalumu (ikihusisha kaya 50 zinazoongozwa na wanaume na saba zinazoongozwa na wanawake) wakati 20% ilikusudiwa ziwe kaya zinazoongozwa na wanawake (kaya 14). Hili lilifanyika ili kuongeza idadi ya kaya zinazoongozwa na wanawake katika utafiti ili kuibua masuala muhimu ya kijinsia na makundi maalumu. Taarifa kutoka kaya 14 zinazoongozwa na wanawake zimehusishwa ili kulinganisha uchambuzi na kaya zinazoongozwa na wanaume na siyo uchambuzi wa jumla wa utafiti.

Awamu ya utafiti shirikishi ilikuwa Februari 2017 na ilihusisha majadiliano ya makundi lengwa 13 na mahojiano ya watu binafsi 12 na kufanya jumla ya watu 92. Makundi tofauti ya kijamii na watu binafsi walichaguliwa mahususi kwa majadiliano na mahojiano ili kuakisi tabia na masuala yanayodhaniwa kuwa muhimu kuchunguzwa zaidi baada ya uchambuzi wa taarifa za matokeo wa utafiti wa awali (Mfano: wajane, wachimbaji, walio kwenye ndoa ya mke mmoja, walio kwenye ndoa ya wake wengi, n.k). Majadiliano ya makundi lengwa yaliundwa kwa kuzingatia viwango vya mazoezi shirikishi (yakihusisha maliasili na misimu ya kuhamahama, uchambuzi wa kazi za msimu, uchambuzi wa wadau na ushirikiano baina ya taasisi mbalimbali). Mahojiano ya wasifu yaliongozwa na muundo wa maswali ambayo yalifumwa kutokana na hali za wahojiwa binafsi ili kusaidia kufahamu maisha ya watu na namna ambavyo mahusiano ya kijinsia na upatikanaji wa rasilimali mbalimbali ulivyobadilika tangu utotoni. Majadiliano ya makundi lengwa yote na mahojiano ya watu binafsi yalihusisha majadiliano huru pia. Utafiti wa mradi ulihusisha mahojiano na viongozi mbalimbali wa serikali za mitaa pamoja na wawakilishi kutoka baadhi ya kampuni za uchimbaji na mashirika yanayofanya kazi Mundarara.

# Eneo na idadi ya watu

Kijiji cha Mundarara kipo katika kata ya Mundarara wilayani Longido, mkoa wa Arusha, kaskazini mwa Tanzania. Mji wa karibu ni mji mdogo wa Longido ambao upo umbali wa kilometa 33 mashariki vikiunganishwa na barabara moja tu ya vumbi. Hapa ndipo yalipo makao makuu ya wilaya ambayo yako chini ya Mlima Longido kandokando ya barabara kuu itokayo Arusha (takribani kilometa 82 kusini) kwenda Namanga (takribani kilometa 28 kaskazini) mpakani mwa Kenya na Tanzania. Hakuna taarifa za ukubwa wa eneo la Mundarara zilizo patikana; eneo la kijiji lilitambulika kutumiwa kwa shughuli kuu mbili za kujipatia kipato ambazo ni ufugaji, na kilimo japo kwa kiwango kidogo. Mundarara ipo umbali wa kilometa 100 tu kutoka eneo maarufu ulimwenguni la Uhifadhi wa Ngorongoro Kreta na wanyama pori huonekana dhahiri katika eneo lote la kijiji ambalo baadhi lipo

ndani ya Eneo Tengefu la Wanyamapori; wilaya pia inahusisha Eneo Tengefu la Uwindaji la Ziwa Natron. Kufuatia taarifa za Ofisi za Madini Kanda (Arusha) mnamo tarehe 11 Octoba 2016, leseni nane (8) za uchimbaji wa madini ya vito (Rubi) katika eneo la Mundarara zilitolewa ingawa leseni moja tu ndiyo ilikua inafanya shughuli za uchimbaji wakati wa utafiti huu.

Mundarara ni kijiji wanachoishi Wamaasai kwa makundi yaliyo tawanyika. Watu katika maeneo tofauti wanaishi pamoja kimila katika maboma (maeneo yenye makazi/nyumba kadhaa na maeneo ya kuchunga mifugo yaliyo zungushiwa vichaka vya miba), ambayo yanaweza kuwa na nyumba hadi 20 ama zaidi. Idadi ya watu katika kijiji ilikua 4,857 waliokua wakiishi katika nyumba 701 hadi kufikia tarehe 12 Octoba 2016.

Asilimia kumi na mbili (12%) ya kaya zilizochaguliwa bila kuzingatia vigezo maalumu wakati wa utafiti wa awali zilikuwa ni kaya zinazoongozwa na wanawake. Kurejea kwenye mapendekezo haya, angalau kaya 84 za Mundarara zilikuwa zikiongozwa na wanawake wakati wa utafiti wetu. Takwimu za utafiti wetu pia zinaonyesha kuwa angalau 54% ya idadi ya watu walikuwa watoto (wenye umri wa miaka 18 au chini), angalau 4% walikuwa wazee (wenye umri wa miaka 65 au zaidi), na 37% tu walikuwa kwenye umri wa kufanya kazi (wenye umri wa miaka 19 hadi 64). Angalau 74% ya wanakaya kutoka kwenye sampuli ya waliohojiwa bila kuzingatia vigezo maalumu walikuwa chini ya umri wa miaka 35, matokeo ambayo ni sawa na wastani wa kitaifa. Jamii ya Mundarara kwa asilimia kubwa inaundwa na kabila moja tu la Wamasai. Ukristo ndiyo dini inayoongoza, na kuna wachache wanaofuata imani za jadi.

Mawasiliano ni magumu Mundarara nzima, ingawa baadhi ya maeneo ya kijiji wanatumia simu za mkononi. Kutokana na kijiji kutawanyika sana, njia/mapitio ni chache sana, barabara ziko chache, hivyo hufanya kusafiri ndani ya kijiji kuwa ngumu na zaidi wakati wa masika (mvua) ambapo baadhi ya mito haivukiki na wanyama wakali wanakuwa wengi pia.

# Historia ya hivi karibuni ya mabadiliko ya uchumi na idadi ya watu

Kijiji cha Mundarara kimepanuka sana ndani ya miongo mitatu iliyopita tangu kuanzishwa kwake kikiwa na idadi ndogo ya jamii za wafugaji wa kimasai waliokuwa wakiishi kuzunguka mgodi mkuu wa Rubi kwenye eneo ambalo kwasasa ndiyo makao makuu ya kijiji. Kabla ya kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa mwaka 1974, kulikua na makazi machache yaliyokuwa yametawanyika na wenyeji wamasai walifanya ufugaji wakuhamahama kwenye eneo hilo. Wakati wa kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa, mipaka ya kijiji iliwekwa na kutambuliwa na kuhamia rasmi kwenye kijiji kuliwezekana kwa ruhusa ya uongozi wa kijiji. Kama matokeo, jamii nyingi zilijenga makazi ya kudumu (maboma) na ufugaji wa kuhamahama ukawa ni wa msimu tu; familia nyingi ziliacha kuhamahama pamoja na badala yake wanaume walienda kuchunga ng'ombe wakati wa kiangazi na wanawake na watoto walibaki kijijini mwaka mzima. Tabia hii ilichochewa na uanzishwaji wa Elimu ya Awali kwa Walioikosa (UPE) kwanzia mwaka 1977.

Kupungua kwa ufugaji wa kuhamahama ulipelekea ongezeko la idadi ya watu na kupanuka kwa eneo la makazi katika kijiji cha Mundarara kwanzia miaka ya 1970. Tangu uchumi wa Tanzania ufungue milango kwa ubinafsishaji kwenye miaka ya 1980, uchimbaji katika eneo la Mundarara ulianza zaidi na kupelekea kuhamia kwa wafanyakazi walio kuja kufanya kazi kwenye mgodi wa kijijj. Ongezeko la idadi ya watu na kukua kwa uchimbaji wa madini na shughuli zinazo ambatana zimezidi kuongezeka hadi leo hii.

# Maisha na mahusiano ya Kijinsia

## Ndoa na hali ya familia

Sehemu kubwa ya aina za ndoa ni za kimila kama ilivyoonekana kwenye utafiti wetu wa awali, ikiwa asilimia 54 (54%) ya ndoa hizo ni za wake wengi, lakini waume zao waliandikishwa kwenye senza

kuwa ni mkuu wa kaya ya mke mwingine. Tulidhani kuwa inawezekana, hata hivyo, baadhi ya wakuu wa kaya wanawake walitengwa na waume zao, na hivyo wakawa kwenye mazingira magumu, lakini hawakusema hivyo wazi kutokana na unyanyapaa kuhusu kujitenga na kupewa talaka. Hali ya ndoa imebadilika sana hivi karibu na kuwa "ndoa za upendo" ambapo vijana wadogo wanaamua ni nani na lini wataoana. Hata hivyo, aina ya 'ndoa ya upendo' ilijikita kwenye dini zaidi (Kikristo)ya mke na mume mmoja, lakini suala la kulipa mahari kwa familia ya mwanamke lilibaki palepale.

## Elimu

Kiwango cha elimu kilionekana kuwa kidogo sana, ikiwa na idadi ndogo ya wanaume na wanawake walioanza shule lakini hawakumaliza elimu ya shule ya msingi. Ilionekana kuwa wanawake wengi walishindwa kumaliza elimu ya shule ya msingi ukilinganisha na wanaume na pia wanawake wengi waliacha shule kutokana na kile kilichoelezwa kuwa ni matokeo ya jamii kutothamini elimu kwa mtoto wa kike likihusishwa na suala zima la wasichana wadogo kuozwa na wazazi wao mapema kwenye umri wa miaka 13 au 14 ili wasiandikishwe shuleni. Kiwango cha chini cha elimu kwa wanaume na wanawake ni kutokana na watu wengi kutosoma (kuacha shule) kwasababu walilazimika kuhamisha mifugo kabla na baada ya uanzishwaji wa vijiji.

## Utajiri na umaskini

Makazi mengi yalikuwa ya kiasili na nyumba zilijengwa kwa na kuezekwa kwa matope au majani; ni baadhi tu ya watu walijenga nyumba za kisasa kwa kutumia matofali hasa Mundarara kijijini (mjini), nyumba zilizo ezekwa kwa mabati na vigae zilikuwa ni chache. Hakuna tofauti kubwa kwenye ubora wa majengo kati ya kaya zinazoongozwa na wanaume na zile zinazoongozwa na wanawake. Kaya nyingi hazikuwa na umeme na chache zilizokuwa nao ni kaya zinazoongozwa na wanaume. Kaya nyingi zinazoongozwa na wanawake zilikuwa na umeme wa jua. Kaya nyingi zilikuwa zinategemea tochi za betri na/au taa za chemli kwa ajili ya mwanga.

Kwa mwaka mzima, chanzo kikuu cha maji kilikuwa ni kutoka kwenye visima vya karibu, ambavyo hutumika na jamii nzima kwa kushirikiano au kulipia. Baadhi ya kaya wanapata maji kutoka kwenye visima vya kina kifupi ambavyo wakati mwingine wanapaswa kulipia ili watumie au kutoka kwenye visima vifupi vya maji. Mara nyingi kaya zinazoongozwa na wanaume wanapata maji kutoka visima vinavyotumiwa na jamii zaidi kuliko kaya zinazoongozwa na wanawake. Kuna idadi kubwa zaidi ya kaya zinazoongozwa na wanawake ambazo wanapata maji kutoka visima vya kulipia, wakielezea matatizo ya ugumu wa kupata maji kwa kaya zinazoongozwa na wanawake masikini. Kaya nyingi hazikuwa na vyoo, na mara chache katika kaya zinazoongozwa na wanaume wanaweza kuwa na choo kimoja.

Punda ndiwo walikua nyenzo kuu ya usafiri. Nyenzo kuu ya usafiri wa kisasa ilikua ni pikipiki ya matairi mawili. Kuna tofauti kubwa sana ya kijinsia kwenye suala zima la umiliki wa nyenzo zote za usafiri, taarifa iliyotokana na utafiti wa awali ilieleza kwamba 20% ya kaya zinazoongozwa na wanaume waliripoti kuwa na usafiri wa pikipiki wakati ni kaya moja tu kati ya zinazoongozwa na wanawake waliripoti kuwa na pikipiki ya matairi mawili. Takriban theluthi mbili ya kaya za sampuli ya wahojiwa bila kuzingatia sifa maalumu kwenye utafiti wetu wa awali walikuwa na simu za mkononi, 21% walikuwa na redio na 7% walikuwa na runinga. Kumekuwepo na tofauti kubwa ya kijinsia kati ya umiliki wa mali kwenye kaya zinazoongozwa na wanawake na zile zinazoongozwa na wanaume, idadi kubwa ya kaya zinazoongozwa na wanawake hazikuwa na simu, redio wala runinga ukilinganisha na kaya zinazoongozwa na wanaume.

Kwa ujumla, taarifa za utafiti wetu wa awali juu ya makazi na vifaa, upatikanaji wa umeme, maji, usafi wa mazingira na usafiri, na umiliki wa mali fulani ilionyesha dalili za viwango vya juu vya umasikini kwenye kaya zinazoongozwa na wanawake. Hii ilidhihirishwa na matokeo ya utafiti shirikishi ambayo yalifafanua maeneo yenye changamoto kwa wanawake.

## Vyanzo vikuu vya kujipatia kipato

Karibu kaya zote wanajihusisha na ufugaji wa jadi kama shughuli yao kuu ya kuishi/kujipatia kipato. Zaidi ya nusu ya wale tuliohojiwa walikuwa wanategemea chanzo kimoja tu cha mapato katika kipindi cha miezi 12 iliyopita na wengine wote walikuwa wanategemea vyanzo viwili tu. Kaya zinazoongozwa na wanaume zina uwezekano wa kuwa na vyanzo viwili vya mapato na kaya zinazoongozwa na wanawake walikuwa na uwezekano wa kuwa na chanzo kimoja tu. Kaya nyingi ziliripoti ufugaji kama chanzo kikuu cha mapato katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, ikifuatiwa na baadhi ya watu kujihusisha na madini, ikiwa ni pamoja na biashara ya madini (udalali), kukusanya kutoka kwenye mabaki ya mchanga, pamoja na uchimbaji wa madini yenyewe. Ilionekana kwamba kaya nyingi walikuwa wakijihusisha na madini lakini haikuwa wazi wakati wa utafiti wa awali.

### *Ufugaji*

Karibu kaya zote wakati wa utafiti wetu waliripoti kwamba walikuwa wakitumia mifugo yao kwa ajili ya kukimu maisha yao ya kila siku, ikilinganishwa na 40% tu ambao walisema kuwa walikuwa wakiuza mifugo hai. Ufugaji wa mifugo una umuhimu mkubwa kitamaduni, na mifugo hutumiwa kama utajiri wa jadi/kimila katika kulipia mahari. Watu wengi huuza mifugo pale tu inapohitajika, wakati wa ukame au shida, badala ya kufugwa hasa kwa ajili ya kuzalisha fedha. Kinyume chake, ikiwa fedha itapatikana kutoka vyanzo vingine kama vile madini au kilimo, basi hakutakuwa na sababu ya kuuza mifugo.

Mgawanyo wa kazi na majukumu kwa kuzingatia jinsia na umri ulionekana dhahiri. Shughuli/kazi za wanawake ni kukamua, kutunza mifugo dhaifu na wagonjwa, na wanaume wanahusika na kuwanywesha maji mifugo, kuhamisha mifugo pamoja na kuchinja na kuuza mifugo. Mgawanyiko huu wote ulikuwepo pia katika kaya zinazoongozwa na wanawake; wavulana walikuwa na wajibu wa kuchunga mifugo, na kwenye kaya 12 za ziada zinazoongozwa na wanawake ambapo watoto wakiume au ndugu wakaribu wakiume walihusika katika kuchinja, kuuza na kununua mifugo hai.

Kimila wanawake hawahusiki sana katika ufugaji tofauti ilivyo sasa, wanawake walianza kushiriki zaidi miaka 30 iliyopita, kwa kuwa watoto wa kiume wameandikishwa shuleni kwa kiwango kikubwa (hivyo ilipunguza uwepo wao kwa ajili ya kuchunga mifugo wakati wa shule). Ilionekana kuwa wanawake wengi walijihusisha zaidi na ufugaji tokea mwaka 2000, kwa sababu ya watoto wote kuandikishwa shuleni jambo lililowafanya wanaume wawe na njia mbadala ya maisha. Hata hivyo, majukumu mbalimbali ya ufugaji, ilibaki kuwa chini ya maamuzi ya wanaume.

### *Mabadiliko ya Maisha*

Ingawa hakuna kaya iliripoti kilimo cha mazao kama chanzo kikuu cha mapato katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, tulijifunza kupitia majadiliano na makundi na mahojiano ya watu binafsi kuwa kilimo cha mazao kilipewa kipaumbele miaka 20 iliyopita kama njia ya kukabiliana na upungufu wa ardhi ya malisho na hivyo kukawepo haja ya kuwa na njia mbalimbali za kujikimu kimaisha. Kilimo sasa kinachukuliwa kama chanzo muhimu cha chakula cha kaya na inachangia kipato cha kaya ikiwa mazao yatauzwa. Lakini kilimo hakitegemewi sana kutokana na ukame wa hivi karibuni; baadhi ya washiriki walisema hawakulima mashamba yao kwa miaka sita iliyopita na baadhi ya watu walielezea kunufaika na kilimo/mazao katika kipindi cha miaka mitatu hadi mitano kabla ya utafiti. Ingawa hakuna mtu anajihusisha na kilimo, ilionekana wazi kuwepo na utofauti mkubwa wa kijinsia kuhusiana na hilo. Wanaume walionekana wakihusika zaidi kwenye kilimo, kupanda/kuotesha na kupalilia. Iliripotiwa kuwa wanavuna pamoja, ingawa wanawake wanaonekana kufanya kazi zaidi; wanawake wengi walisema kuwa baada ya mavuno, mazao yote yanamilikiwa na wanaume na wanawake walikuwa wakipewa mahindi kidogo tu ya kusaga kwa ajili chakula cha watoto.

Mwenendo/haja ya kuwa na njia mbadala wa maisha mbali na njia za kimila (ufugaji) tu ulionekana dhahiri. Uchimbaji wa madini ulileta fursa mpya kwa jinsia zote mbili na kwamba wanawake na wanaume wanajihusisha na biashara ndogondogo. Wakati huo huo, ukame wa muda mrefu kwa

miaka ya hivi karibuni ulionesha changamoto ya maisha ya kawaida, na watu wengi sasa wanategemea zaidi kipato kutokana na shughuli zinazohusiana na madini wakati kilimo kinapotea na ubora wa malisho unapotea pia kutokana na ukosefu wa mvua na kuongezeka kwa idadi ya watu na mifugo. Hii inachangia mazingira ya migogoro juu ya madini na malisho na pia wanawake kulemewa zaidi na majukumu kama vile mgawanyo wa majukumu kijinsia utakavyokuwa mbaya zaidi.

### Mahusiano ya kijinsia

Kama ilivyoonekana, kumekuwepo na taratibu za kimila na kidesturi juu ya mgawanyo wa majukumu kwa kuzingatia jinsia kwenye kaya za Wamasai, huku wanawake wakionekana kuhusika zaidi na majukumu ya nyumbani ndani na nje ya boma. Maamuzi ndani ya kaya, ikiwa ni pamoja na mgawanyo wa shughuli/majukumu ya kila siku kuhusu ufugaji na kilimo cha mazao hufanywa na wanaume. Hata hivyo, mabadiliko kidogo yanaletwa na 'ndoa za upendo' (ingawa bado ni chache) na kwenye ndoa za mume/mke mmoja, na hii huenda ni kwasababu ya kuhubiriwa makanisani juu ya haki za mwanamke. Wanawake na wanaume walioko kwenye ndoa ya mke/mume mmoja waliripoti kuwa angalau mke anahusishwa na hushauriana katika maamuzi ya kaya.

Mtazamo wa kuongezeka kwa utajiri kutokana na kuwa na mifugo wengi zaidi ulionekana kuwa sababu mojawapo ya wanaume kuoa wake wengi, kwani kuwa na wake wengi inawasaidia wanaume kuwa na wafanya kazi wengi zaidi kutunza mifugo yao na kushirikiana kazi/majukumu mbalimbali. Hata hivyo wanawake wengi walio kwenye ndoa ya wake wengi waliripoti kuwa kiuhalisia mgawanyo wa majukumu kati ya wake wenza haulingani kutokana na kile kilichadaiwa kuwa mume anamppendelea mke mmoja (mara nyingi yule mdogo wa mwisho kuolewa) jambo ambalo limeonekana kusababisha migogoro kati ya wake wenza hao.

Majukumu ya wanawake yameendelea kuongezeka maradufu kutokana na suala zima la kujihusisha na njia mbadala ya kujipatia kipato: wanahusika kwenye uchungaji wa mifugo na wakati huo wanawajibika na majukumu ya kaya. Wakati ilionekana kuwa wana maamuzi juu ya fedha wanazopata kutokana na kujihusisha na shughuli za kujipatia kipato, kiuhalisia hili liliwezekana tu kama fedha iliyopatika ni kiasi kidogo sana cha fedha na kwamba wanawake walipaswa kutumia fedha hiyo kwa ajili ya familia nzima na siyo kwa ajili yao wenyewe, hasa kwa ajili ya watoto, ada ama mahitaji mengine. Katika kaya nyingi walio kwenye ndoa hapakuwa na wanawake waliodai kupata fedha katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, hii imewafanya wanawake kwenye kaya kulazimika kuwategemea waume zao kwa ajili ya mahitaji yao ya kifedha ya kila siku.

Ukosefu wa rasilimali fedha ilionekana kuwa moja ya changamoto kubwa kwa wanawake kwa ujumla. Ingawa inaonekana kwamba ndugu wa kiume wa wanawake, hasa watoto wao wa kiume, waliwasaidia mara nyingi sana na kuendelea kuwasaidia katika maisha yao yote, lakini ukosefu wa vitega uchumi na ulinzi wa mgawanyo huru, na utegemezi wao wa kiuchumi kwa wanaume, vimeongeza ugumu kwao kuachana na waume zao pamoja na unyanyapaa juu ya kutengana na talaka; pia hali hiyo ilisaidia kufafanua sababu za wanawake wajane kuwa kwenye kundi la watu walio kwenye mazingira magumu zaidi, hasa wakiwa na watoto wasio na rasilimali za kutosha na bila msaada wa kutosha.

Wakati wanawake wengi walilalamikia suala la majukumu mengi waliyonayo, unyanyasaji wa kila siku na ukosefu wa vitega uchumi/mali, ushiriki finyu kwenye siasa; ni wanaume wachache tu ndiwo waliokubaliana na haya.

## Uchimbaji Mundarara

Uwepo wa madini ya rubi Mundarara umetoa fursa muhimu kwa wanajamii wanaojitahidi kujihusisha na njia mbadala za kipato, na ilionekana kuwa kila kaya kwa namna moja au nyingine inajihusisha na madini.

## Makampuni ya uchimbaji madini

Kwa miaka ya hivi karibu, kampuni mbili za madini zimekuwa zikifanya kazi ya uchimbaji wa ruby. Mundarara Ruby Mining Company (MRMC), ina historia ndefu; Wadau wa sasa katika kampuni hiyo ni Serikali ya Tanzania, mmiliki wa leseni ya eneo la MRMC na Mwendeshaji. waendeshaji wamekuwa wakibadilika mara kwa mara; waendeshaji wa sasa wamedumu kwa miaka mitano. Kampuni ya pili, ni Paradiso Minerals, hii ilianzishwa na mkurugenzi wa zamani wa kampuni ya Mundarara Ruby Mining (MRMC) kwa takriban miaka minne kabla ya utafiti wetu Mundarara. Iliacha kufanya kazi kwa sababu ya migogoro na wanakijiji na ilikuwa katika mchakato wa kujenga nyumba za walimu ili kurudisha uhusiano bora na jamii. Kampuni ya tatu ni Mundarara Village Ruby Mine.Hii ilianzishwa na serikali ya kijiji mwaka 2009 na kuanza kufanya kazi mwaka 2010 kwa ushirikiano na mwekezaji wa Kiarabu lakini ilisimama kufanya kazi mwaka 2015. Kampuni hii iko chini ya STAMICO, chombo kilichoundwa na serikali ili kusaidia wachimbaji wadogo. Kampuni ya kijiji ilikodisha kwa waendeshaji binafsi ambao walipaswa kuipa serikali ya kijiji asilimia fulani ya faida yao, na jengo la ofisi ya kijiji na vyoo vilijengwa kwa mapato kutokana na madini ya kampuni ya kijiji. Hata hivyo, haikufanya kazi miaka miwili iliyopita kabla ya utafiti wetu kutokana na kukosekana kwa wawekezaji wenye mitaji ya kutosha.

## Mchango wa madini kwa ustawi wa/maisha ya jamii

### *Kazi*

Wahojiwa wa makundi na watu binafsi wakati wa utafiti wetu, ambao ni pamoja na watu kadhaa wanaojihusisha moja kwa moja kwenye uchimbaji madini katika kampuni ya MRMC, walilalamika juu ya mishahara midogo na kuhusu ucheleweshaji wa malipo na mazingira magumu ya kufanya kazi; kwa ujumla wanaona kuwa kuna haja ya kuboresha mazingira ya kazi na kutaka kupewa kazi zaidi, ikiwa ni pamoja na ajira katika nafasi za juu za usimamizi. Kulikuwa na malalamiko kuhusu uwepo wa wafanyakazi wengi kutoka nje ya kijiji na hivyo kuwa ngumu zaidi kwa watu wa ndani/jamii kupata kazi kwenye kampuni hii; waombaji walipaswa kupitia serikali ya kijiji ili kupendekezwa au kujaribu kupata kazi moja kwa moja kwenye kampuni kwa kutoa rushwa. Hata hivyo, wakati MRMC ilikiri kuwa asilimia 50 ya wafanyakazi wake wanatoka nje (wenye ujuzi na uzoefu wa madini), kampuni hiyo imesema kuwa huchukuwa watu 40 wa jamii ya Mundarara wasiojua kusoma na kuandika na kuwafundisha kazi, ikiwa ni pamoja na asilimia 50 ya wasimamizi. MRMC haijawaajiri wanawake, moja ya sababu ni kile kinachodaiwa kuwa hawawezi kufanya kazi hiyo, na sababu ya pili ni madai kwamba ni ili kuzuia ubakaji na unyanyasaji dhidi ya wanawake ambao wangeweza kupewa kazi za ofisi au za nyumbani. Wafanyakazi wote wanaoishi ndani ya eneo la mgodi hawaruhusiwi kutoka nje na wanawake kutoka nje hawaruhusiwi kuingia ndani.

### *Uchambuzi wa madini kutoka kwenye mabaki ya mchanga na biashara ya Madini*

Kulikuwa na mgawanyo wazi wa majukumu kijinsia kwenye uchimbaji madini pamoja na shughuli za zinazohusiana; wanawake wengi wanaokota madini kutoka kwenye mabaki ya mchanga na wachache wao tu ndiwo wanaohusika katika biashara ya madini na udalali. Kila siku, wanawake na wanaume wanaenda kuokota madini kutoka kwenye mabaki ya mchanga unaotolewa na kampuni ya MRMC; wanachukuwa mawe yanayoonekana kuwa na madini ndani yake na kujaribu kuwauzia madalali wakubwa wa kiume kijijini. Watu wengi wanaojishughulisha na kazi hii hawafahamu thamani ya madini wanayopata na hivyo hudanganywa. Wanawake wanapata kiasi kidogo zaidi cha fedha wanapouza madini waliyookota. Kwa upande mwingine, uchakataji na biashara ya madini vinaonekana kuwa na faida kubwa inayowanufaisha zaidi matajiri na wote walio na mahusiano na masoko makubwa na hivyo inawaongezea utajiri na mali. Pia kumekuwepo na migogoro inayohusiana na utoaji wa madini kutokana na kwamba watu wote wanagombania rasilimali finyu inayopatikana na wanawake walikuwa wananyanyaswa na kudhalilishwa. Watu wengine pia wanadhani kwamba kampuni ya MRMC ilikuwa inawadanganya kwa kutoa mchanga ambao hauna

madini ndani yake, lakini hii ilifafanuliwa na waendeshaji wa kampuni kuwa ni kutokana na kushuka au kutokuwepo kwa uzalishaji kwenye kampuni.

### Athari za Uchimbaji Madini

Palionekana kuwa na hisia kinzani baina ya watu katika kijiji cha Mundarara juu ya madhara ya uchimbaji kwao na kwa kijiji. Ingawa wengine walifurahia faida za kifedha, wengine wanaona kwamba migogoro inayohusiana na madini ambayo pia ilisababisha vifo vya watu na kupoteza ardhi imepelekea hasara kwa jamii. Hata hivyo, ni wazi kwamba madini hayo yamechangia sana kuboresha maisha ya watu, kwa mfano wakati wa utafiti wetu tuliona majengo mengi mapya yaliyoongezeka. Watu wengi pia walisema kuwa wangependa kuona mahusiano mazuri zaidi kati ya makampuni ya uchimbaji madini na wanakijiji kwa njia ya mikutano, kuboresha mazingira ya kazi na miradi halisi mbalimbali ya kijamii.

Ilikuwa ni vigumu kufahamu kama maendeleo ya uchimbaji madini yatakuwa tishio kwa ardhi ya watu wa Mundarara kwa miaka ijayo kutokana na uchimbaji madini kuwa wa kiwango kidogo wakati wa utafiti wetu. Hakuna kampuni nyingi/wawekezaji hawajajitokeza kuwekeza zaidi huko Mundarara ili kuendeleza uchimbaji. Ilionekana pia kuwa watu wa Mundarara walitaka kupata faida zaidi kutokana na madini ya rubi, hivyo wakaamua kuanzisha mgodi wa kijiji. Kitendo cha Makampuni ya madini kuchukua mashamba na maeneo ya malisho, na ukosefu wa vyeti vya kimila vya umiliki wa ardhi, pamoja na migogoro ya mara kwa mara na unyanyasaji unaosababishwa na madini, yote yanapelekea hofu na wasiwasi kwa watu wengi wa eneo hilo. Hata hivyo umuhimu wa madini kwenye kaya nyingi unaonekana pale tu kilimo kinapoathiriwa na ukame pamoja na changamoto katika ufugaji. Imethibitika kuwa mchango wa madini ni mzuri na ni kipaumbele kwa watu wengi.

## Utaratibu na mpango wa ugawaji wa ardhi

### Wanyamapori na Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi

Kama ilivyoelezwa huko juu, Mundarara ilikuwa sehemu ya Eneo la Usimamizi wa Wanyama Pori (WMA), na angalau kampuni moja ya uwindaji ilifanya kazi katika eneo hilo wakati wa utafiti wetu; mashambulizi ya wanyamapori yaliripotiwa kuwa ni ya mara chache sana. Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji (VLUP) ulianzishwa Mundarara mwaka 2012, sehemu ya mpango wa matumizi bora ya ardhi ni ili kupunguza migogoro kati ya wafugaji na wanyamapori. Ndani ya mpango matumizi bora ya ardhi (VLUP), unaonesha kuwa ardhi yote ya kijiji imepangiwa matumizi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji na makazi, pia imetenga maeneo ya misitu na madini, ingawa rasilimali kama vile kuni zinaweza kukusanywa na watu bila malipo kwenye eneo lolote. Watu wengi walielezea wasiwasi wao juu ya udogo wa ardhi iliyosalia kwa ajili ya kuendeleza makazi na kilimo. Hata hivyo, inaonekana wazi kwamba mpango wa matumizi bora ya ardhi (VLUP)unalenga hasa (na muhimu zaidi) kwa wafugaji kwa ajili ya kuweza kulinda na kusimamia ardhi ya malisho/kufugia.

### Usimamizi wa ardhi na mitazamo kuhusu sheria

Kabla ya uanzishwaji wa vijiji, ardhi huko Mundarara ilikuwa kubwa na ilisimamiwa kwa njia za kimila zaidi. Hata hivyo, ujio wa taasisi za kisheria umekuja na nguvu zaidi kuzidi njia za kimila. Mashamba na maeneo ya makazi sasa yanasimamiwa na kanuni za kisheria na yeyote anayetaka aina yoyote ya ardhi atatakiwa kuomba kwa kupitia serikali ya kijiji. Eneo la malisho linasimamiwa kwa ushirikiano kati ya serikali ya kijiji na Ilaigwanak ambayo ni halmashauri ya kimila ya Wamasai pamoja na maelekezo yaliyoko kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Uamuzi wa jamii kwa ujumla katika kijiji cha Mundarara unatawaliwa na wanaume na takriban viongozi wote wa serikali ya mtaa ambao wako kisheria ni wanaume. Wanawake wachache walioko

kwenye serikali ya Kijiji (kama inavyotakiwa kisheria) kwa ujumla hawatambuliwi na wanawake wenzao kama wenye msaada kwao.

Uelewa wa jamii kuhusu sheria za Tanzania juu ya umiliki na usimamizi wa ardhi unakanganywa sana, ikiwa ni pamoja na uelewa mdogo wa sheria kwa ujumla na mitazamo hasi kuhusu haki za ardhi kwa wanawake na haki za umiliki wa madini.

## Upatikanaji wa ardhi ya makazi na mashamba

Kihistoria watu walijichukulia tu kiasi cha ardhi yoyote waliyoitaka kwa ajili ya makazi na mashamba. Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, na thamani ya ardhi kuendelea kuongezeka, imekuwa vigumu kujichukulia eneo la ardhi bila kufuata utaratibu wa kisheria. Malalamiko yalielekezwa kwenye ucheleweshwaji wa mchakato wa kupewa ardhi, kuwepo kwa haja ya kufuatilia mara kwa mara, na ugumu wa watu masikini kupata ardhi. Kukosa ufafanuzi kuhusu hali halisi na kiasi cha ada kinachohitajika kulipwa ili kupata ardhi, wasiwasi mkubwa ni kwamba upatikanaji wa ardhi kwa kufuata utaratibu wa kisheria hasa kwa watu masikini na wanawake, wanaweza kuwa kwenye hatari ya msukumo wa kulipa "kwa njia fulani" tofauti na fedha.

Kuna ukosefu wa maelezo sahihi (ufafanuzi) kuhusu hati zinazohusiana na ardhi. Hakukuwa na kaya iliyoripoti na nyaraka yoyote ya umiliki wa ardhi. Hata hivyo, umiliki ulitafsiriwa kwa njia tofauti. Wakati watu wengine katika mahojiano na makundi na watu binafsi katika utafiti wetu walisema wanazo risiti halali za umiliki wa ardhi kimila, wengine walisema wanamiliki ardhi zao tu bila nyaraka zozote na hata hawaoni haja ya kuwa na nyaraka hizo.

Baadhi ya wahojiwa wetu kwenye makundi na watu binafsi waliripoti kununua ama kukodisha eneo kwa ajili ya kilimo cha mazao. Ilionekana kuwa baadhi ya watu matajiri walitoa maeneo yao yalimwe na watu wanaowachungia mifugo; (mtu anafuga mifugo ya tajiri na malipo ni kupewa shamba alime). Hata hivyo, hakuna hata mmoja kati ya wale waliohojiwa kwenye utafiti wetu wa awali walioripoti kuwa na ardhi isiyokuwa ya makazi walioipata kwa kukopa au kukodisha.

## Migogoro ya Ardhi

Aina nyingi ya migogoro ya ardhi ni ya mipaka inayosababishwa na watu kupanua mashamba yao na kuingia eneo la/ardhi ya jirani zao na migogoro ya kuhamahama kwa mifugo. Wanawake na wanaume huenda kutatua migogoro yao ya ardhi kwenye baraza la ardhi la usuluhishi la kijiji; wanawake wajane ambao maeneo/ardhi yao yamechukuliwa na watu wengine ndiwo wengi. Migogoro na makampuni za uchimbaji madini inatatuliwa na serikali ya kijiji kwa njia ya kujadiliana na makampuni na siyo kwa kupitia baraza la ardhi la usuluhishi. Migogoro kuhusu matumizi ya eneo la malisho na ya kuhamahama kwa mifugo ambayo imekuwa ikiongezeka mara kwa mara katika miaka ya hivi karibuni kutokana na ukame, haikutatuliwa na baraza la ardhi la usuluhishi badala yake ilitatatuliwa na Ilaigwanak (uongozi wa kimila).

## Upatakanaji wa ardhi kwa wanawake kwa mifumo ya kisheria

Mfumo wa kisheria wa ugawaji wa ardhi na ukuwaji wa soko la ardhi vinatoa fursa sawa ya kupata na kumiliki ardhi kwa wanawake na wanaume wa Mundarara kama ilivyo nchini kote. Hata hivyo, kuna changamoto nyingi za kimuundo ikiwa ni pamoja na kanuni za kimila ambazo zinazuia wanawake kupata ardhi. Pia ilionekana kuwa wanawake wengi hawatambui haki zao na hawafahamu mchakato sahihi wa kuomba ardhi. Wanawake wanalalamikia suala la maslahi yao kutozingitiwa na kupewa kipaumbele na serikali ya kijiji inayoongozwa na wanaume, wengine hawafahamu waende kwa nani kudai ulinzi wa haki; wengine walidhani watapata kusaidiwa na serikali ya kijiji, au huenda maslahi yao hayatapewa uzito endapo hawatasaidiwa na wanaume. Zaidi ya hayo, wanawake wengi, na hasa wajane, hawawezi gharama zinazohusishwa na kuomba ardhi, wala kununua au kukodisha ardhi kwa matumizi yao wenyewe.

Swali linalojitokeza ni kwamba, je utajiri na fedha ni vya muhimu zaidi kuliko usawa wa kijinsia katika kuwezesha upatikanaji wa ardhi (na mifugo) Mundarara kwa wakati huu?. Kama ndivyo, au ikiwa mambo yataendelea kama yalivyo sasa, basi kuwawezesha wanawake kiuchumi, kwa mfano kwa kuhakikisha kuwa wanaweza kufaidika kwa kiwango kikubwa kutokana na madini, itakuwa ni njia bora na sahihi ya kuwasaidia wanawake kupata usalama na umiliki wa ardhi, na, kwa muda mfupi, kutaongeza ushawishi ndani ya serikali ya mtaa juu ya masuala ya usimamizi wa ardhi.

## Usimamizi wa ardhi/eneo la malisho

Matokeo ya ongezeko la kasi ya urasimishaji wa ardhi kuanzishwa kwa vijiji na mabadiliko mengine kama vile ongezeko la idadi ya watu na kuanzishwa kwa elimu ya msingi kwa waliokosa (UPE); Wamasai sasa wamepunguza kuhamahama na tuliambiwa mifugo inahama tu kwa nyakati maalum kwa mwaka, na wanaume ndiwo uhama nayo na kuwaacha wanawake na watoto nyumbani.

Kama ilivyoelezwa juu, usimamizi wa eneo la malisho ulifanywa kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora wa ardhi ya kijiji cha Mundarara na sheria zinazohusiana na mpango huo kwa ushirikiano wa serikali ya kijiji na Ilaigwanak. Wahojiwa wa makundi na watu binafsi wakati wa utafiti wetu walisema; *"kwa kuondolewa kwa umiliki wa kimila umewafanya viongozi wa mila/ilaigwanak kupoteza nguvu tofauti na walivyokuwa hapo mwanzo*". Hata hivyo, wakati upatikanaji wa eneo la malisho na utaratibu wa kuhamisha mifugo kuonekana kushika kasi zaidi, Ilaigwanak bado wameonekana kuwa na nafasi kubwa ya kutatua migogoro inayohusiana na kuhamisha mifugo kutokana na mamlaka yao kutokuwa na mipaka hivyo uongozi wao bado unaheshimiwa.

Hata Ilaigwanak imetawaliwa na wanaume tu na hakuna wanawake; hivyo basi, maamuzi yote kuhusu kuhamisha mifugo na ufugaji (kuchunga) yanafanywa na wanaume, na mara nyingi wanawake wanapewa taarifa ya muda mfupi sana kuhusu wanaume kuhama na mifugo.

### Upatikanaji wa eneo la malisho na kubadilika kwa mifumo ya kuhama

Kabla ya uanzishwaji wa vijiji, maeneo ya malisho yalionekana kuwa ya kutosha na yenye ubora mzuri. Hata hivyo, mvua zisizotabirika, kuongezeka kwa idadi ya watu na ongezeko la kilimo cha mazao katika kipindi cha miaka 20 iliyopita imesababisha migogoro mingi juu ya malisho ndani na karibu na Mundarara. Kuongezeka kwa idadi ya mashamba na makazi, pamoja na kuwepo kwa makampuni ya madini, imeongeza umbali wa watu kutembea ili kufikia maeneo ya malisho (kufugia). Ardhi ya jamii inatumiwa na watu wote wa vijiji vya jirani kwa ushirikiano baina ya serikali za vijiji vya jirani na viongozi wa kimila.

Wakati mifugo midogo (mbuzi na kondoo) wanaweza kushiba kwa malisho kidogo sana na vichaka vikavu, mifugo wakubwa kama vile ng'ombe wanategemea malisho ya kutosha (uwepo wa majani ya kutosha) kwa ajili ya kuishi. Watu wengi walikuwa wanategemea maeneo makubwa ya ardhi ya jamii kwa ajili ya maisha. Ni wachache tu wenye idadi ndogo ya mifugo wanaofugia kwenye mashamba/maeneo yao. Inaonekana kuwa watu wengi wanawalipa baadhi ya watu kama vibarua kwa ajili ya kuchunga na kuhamisha mifugo nyakati za misimu mirefu, hii ni kwa sababu wanaume waliokuwa wakichunga mifugo wamejihusisha zaidi na biashara ya madini.

Sehemu kubwa ya eneo la malisho Mundarara linatumika na watu wote wakati wa mvua lakini baadhi ya maeneo yalitengwa ili yatumike na mifugo dhaifu na midogo isiyoweza kuhama wakati wa ukame. Ilaigwanak na serikali ya kijiji wameweka utaratibu wa kuwajulisha watu wakati maeneo yaliyotengwa yatakaporuhusiwa kuchunga kipindi cha ukame ambapo pia wanaruhusu kuhama kwa mifugo mingine. Endapo mtu yeyote atavunja utaratibu uliowekwa kwa ajili ya maeneo yaliyotengwa kutumika na mifugo dhaifu na wadogo wasioweza kuhama, watalazimika kulipa faini.

Umbali wa kuhamisha mifugo na muda mrefu wa kukaa huko na mifugo, hupelekea waliohamisha mifugo kulazimika kukaa huko kwa kipindi kisichopungua miezi mitano. Hapo awali, wafugaji walihamia maeneo ya karibu ambapo waliweza kuhama na famialia zao na kuanzisha makazi mapya.

Hata hivyo, kuhamahama kulikuwa kwa mara kwa mara nyakati za ukame na ni vijana wadogo ndiwo walihusika zaidi.

Migogoro juu ya maeneo ya malisho imeongezeka sana kati ya wanakijiji wenyewe na vijiji vya jirani. Ukweli ni kwamba maeneo ya malisho yanatumiwa na mifugo na wanyamapori na hivyo imeongeza migogoro zaidi kwenye ardhi; kwa mfano, ikiwa maeneo ya madini yanazuia upatikanaji/kufikiwa kwa maeneo ya malisho ya hapo awali, watu wanaweza kukabiliwa na hatari katika kujaribu kupeleka mifugo maeneo mapya kutokana na uwepo wa wanyamapori wakali/hatari. Njia ya kawaida ya kutatua migogoro ni kupitia mazungumzo kati ya watu binafsi au kupitia mikutano ya kijiji. Inaonekana kuwa kutokana na kuongezeka kwa migogoro ya ardhi watu sasa wanaona kuna haja/sababu ya msingi ya kujaribu kupunguza migogoro hiyo kwenye maeneo ya malisho ambapo kama haitawezekana basi wataamua kujiwekea mipango binafsi.

## Hitimisho

Mabadiliko ya tabia nchi pamoja na ongezeko la idadi ya watu, vimechangia sana kutotabirika kwa ufugaji huko Mundarara kuliko ilivyokuwa hapo awali. Kuwepo kwa kilimo (licha ya ukame wa miaka michache iliyopita) imepelekea ardhi kurasimishwa zaidi na usimamizi umezigatiwa pia. Uanzishwaji wa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi umetenga maeneo ya malisho na kupunguza upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya upanuzi wa makazi na kilimo. Wakati huo huo, watu wengi wameanza kujaribu njia mbalimbali ya kuendesha maisha, madini tu peke yake ni njia mojawapo ingawa upanuzi wa maeneo ya madini pia umesababisha ugumu kwa upatikanaji wa ardhi ndani ya kijiji.

Ingawa kazi kadhaa zilipatikana, wanaonufaika zaidi kwenye madini ni wanaume wanaouza na madalali wa madini ambao wengi wao wametajirika kutokana na kuuza madini ya rubi. Uchimbaji pia umewapa wanawake (na hasa wajane) fursa kadhaa za kupata kipato kidogo cha fedha kwa kukusanya mabaki ya madini kutoka kwenye mchanga unaotolewa na kampuni ya uchimbaji. Hata hivyo, faida kwa wanawake siyo kubwa kutokana na kutofahamu thamani ya madini wanayookota, pamoja na ubaguzi wa kijinsia ambao unawakabili wanawake wakati wanapojaribu kukusanya mabaki ya madini. Ubaguzi huu ni udhalilishaji wa maneno na wa moja kwa moja kama walivyotutaarifu wakati wa utafiti wetu.

Ijapokuwa shughuli za madini zimechangia uchumi wa wanajamii wa Mundarara, baadhi ya masuala mabaya pia yalionekana. Iligundulika pia kuwa watu wengi hawafurahiswi na ushirikiano uliopo kati ya makampuni ya madini na kijiji cha Mundarara, na kwamba kuna haja ya kuboresha mahusiano hayo kwa kushauriana, kulipa fidia na kuhakikisha kuwa jamii inanufaika zaidi. Masuala haya yamechangia kujenga chuki, vurugu na maandamano.

Kitendo cha wanaume wengi kujihusisha na shughuli za madini na mwelekeo mzima wa maisha kwa ujumla vimepelekea wanawake wengi kuwa na majukumu mengi zaidi nje ya kaya. Wakati wanawake wengi wanahusika na kuchunga na wengine wapo kwenye shughuli mbalimbali za kujipatia kipato, bado wanawakwe wanahusika kukamilisha majukumu yote ya nyumbani na hawaruhusiwi kufanya maamuzi juu ya fedha wanazojitafutia. Iligundulika kuwa maamuzi yote ndani ya jamii yanafanywa na wanaume licha ya baadhi ya wanawake kuwa na wajumbe kwenye serikali za vijiji kama sheria ilivyoagiza. Hata hivyo, kuna baadhi ya mabadiliko yanayoanza kuonekana kwenye baadhi ya kaya. Kwa mfano, ingawa ndoa ya wake wengi inaonekana kuongoza zaidi kuliko ndoa ya mume/mke mmoja, ndoa ya mume/mke mmoja zinakuwa kwa kasi na kwamba maamuzi yanaonekana kuwa shirikishi baina ya mume na mke katika ngazi ya kaya, mfano kuhusu bajeti na matumizi. Hata katika ndoa za wake wengi, inaonekana kwamba baadhi ya wanawake wanayo nguvu na mamlaka zaidi kuliko wengine, na tuliambiwa kuwa wake (mke) waliopendwa na waume zao wanashiriki kwenye maamuzi ya kaya na pia wana haki zaidi kuliko wengine. Tulitambua pia kuwa kile watu wanachosema wamekifanya ukilinganisha na ukweli unakuta kwamba kiuhalisia siyo kweli/sawa. Baadhi ya wanaume wengine walikuwa tayari kubadilika na kuunga mkono jitihada zote

zinazotetea haki za wanawake na kunufaisha familia nzima, wakati huohuo wakiheshimu mila na desturi zilizoko.

Kuongezeka kwa urasimishaji na usimamizi wa ardhi kinadharia imetoa fursa sawa ya wanawake wa Mundarara kuwa na na haki sawa za kupata ardhi na kuwa na umiliki wa pamoja wa ardhi ya kaya na hivyo imewahakikishia usalama wa ardhi zao. Hata hivyo, kiuhalisia, tulitaarifiwa mara kwa mara kwamba wanaume hawaruhusu wanawake kumiliki aina yeyote ya ardhi na kwamba serikali ya kijiji pia ilikuwa ikiwapa ardhi wanawake wajane ambao wana watoto wa kiume wenye umri wa zaidi ya miaka 18 ili waweze kusimamia hizo ardhi. Zaidi ya hayo, mifugo yote inamilikiwa na wanaume tu. Kwa mali hizi mbili muhimu zilizoko mikononi mwa wanaume, imewafanya wanawake washindwe kujitegemea na kuzalisha mali au kuchangia kipato kwenye uchumi wa kaya. Wajane (na wanawake wachache walioachika), hasa wale walio na watoto wa kuwalea, pia wanaonekana kuachwa na mali ndogo sana/isiyotosheleza, ugumu wa kupata rasilimali na kukosa msaada wowote kutoka kwa wanaume. Ingawa tulikutana na wanaume wachache ambao ni maskini sana, bado wanawake wako katika kundi la watu walio kwenye mazingira magumu zaidi Mundarara.

Mabadiliko ya tabia nchi na hali ya hewa, ukame na uchimbaji wa madini vimesababisha migogoro juu ya uhaba wa maeneo ya malisho na rasilimali maji. Vitisho hivi vya nje vimebadilisha maisha ya wafugaji na mgawanyo wa majukumu kwa kuzingatia jinsia Mundarara, wakati vitisho vya ndani ambavyo vinawakumba wanawake wengi wa jamii hii vilionekana kuwa vigumu sana kuvikabili. Kuelimisha wanawake na wanaume kuhusu haki za ardhi, kutoa mafunzo ya uongozi kwa wanawake, na kuanzisha vikundi ili kuwasaidia wanawake kurahisiha upatikanaji wa ardhi na mifugo ni mapendekezo yaliyopewa kipaumbele kama baadhi ya masuluhisho kwa matatizo haya. Majukumu mengi yanayotekelezwa na wanawake yanabaki kuwa kikwazo kikubwa kufikia malengo. Kuweka mazingira ya jamii nzima kuwa na jukwaa la kukutana na kujadili masuala muhimu ya ardhi na maliasili kwa njia ya kushirikiana itasaidia kushughulikia masuala mbalimbali ambayo pia yalijitokeza wakati wa uatafiti wetu ambayo ni masuala ya ardhi, jinsia, uchimbaji wa madini na ufugaji na hivyo kusaidia kuleta maendeleo endelevu Mundarara. Mijadala hiyo ijumuishe wanaume na wanawake, vijana na wazee, matajiri na maskini, na msaada maalum kwa makundi ya watu walio katika mazingira magumu ili kuhakikisha kuwa mahitaji yao yanasikika, yanatambulika na kushughulikiwa ipasavyo.

mokoro

HakiMadini